

'Wakaguzi wa ndani zingatieni miongozo'

Mwandishi Wetu, Mwananchi
mwananchi@mwananchi.co.tz

Dar es Salaam. Wakaguzi wa ndani wametakiwa kuzingatia sheria, kanuni, viwango na miongozo ya Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) wanapofanya ukaguzi kwenye miradi na mifumo ya Teknolojia ya Habari na Mawasiliano (Tehama) ili watoe ushauri wenye tija kupitia taarifa zao za ukaguzi.

Mkaguzi Mkuu wa Ndani Msaidizi kutoka Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wa Serikali, Paison Mwamnyasi alisema hayo hivi karibuni, katika ufunguzi wa awamu ya pili ya mafunzo maalumu kwa wakaguzi hao kutoka halmashauri na tawala za mikoa 13 za Tanzania Bara.

"Ukielewa mifumo inavyofanya kazi, unaweza kukagua ipasavyo na tutaepuka kutaja majina ya watu katika taarifa za ukaguzi, sisi wakaguzi tunatambua kuwa miongozo ya ukaguzi inaeleza kutokagua sehemu ambayo hauna uelewa nayo kwa kuwa unaweza kutoa maoni na ushauri ambao hauna tija," alisema.

Mkurugenzi wa Udhhibiti na Usalama wa Tehama kutoka e-GA, Sylvani Shayo alisema kwa kushirikiana na Ofisi ya Mkaguzi Mkuu wa Ndani wanaendelea na jitihada za kutoa mafunzo kwa wakaguzi ili waweze kufanya ukaguzi katika eneo la Tehama kwa ufanisi.